# USCRI JUA HAKI ZAKO

## Mwongozo kwa Wahamiaji

Bila kujali hali ya uhamiaji, batu bote mu inchi ya Marekani bako na haki zenye zinalindwa na kuhakikishwa na Katiba. Hii mwongozo imetayarishwa kwa kujulisha batu benye habako banainchi ba Marekani kuhusu haki zao za kisheria mu hali mbalimbali wakati banakutanana na maafisa wa sheria na maafisa wa uhamiaji.

Sheria za majimbo **fulani** zinaweza kutofautiana. Sheria tofauti zinatumika mu **vituo ya ukaguzi** na wakati ya kuingia Marekani kupitia fasi rasmi za kuingilia mu inchi, sawa vile ku mipaka na ku viwanja ya ndege.

**Hii maelezo imetolewa kwa malengo ya elimu na haipashwi kutumiwa ku nafasi ya msaada wa kisheria. Kama weye ao mutu mwenye unajua anahitaji msaada wa kisheria, tafazali wasiliana na mwanasheria.**

## MAAFISA WA KUTEKELEZA SHERIA

### MAREKANI Idara ya Utekelezaji wa Sheria za Uhamiaji na Foroza (ICE)




- ICE inafanya misako mu nyumba, fasi za kazi, na inashirikiana na polisi fulani ba mu eneo.
- Uko na haki ya kubakiya kimya.
- Uko na haki ya kukuwa na mwanasheria, lakini ICE hailazimike kukupatia mwanasheria.

### Kitengo cha Uchunguzi wa Usalama wa Taifa (HSI)




- HSI inachunguza uhalifu wa kimataifa na inafanya misako mu fasi za kazi.
- Uko na haki ya kubakiya kimya.
- Uko na haki ya kukuwa na mwanasheria, lakini HSI hailazimike kukupatia mwanasheria.

### Polisi wa Jimbo / Polisi wa Eneo




- Kwa kawaida polisi iko na jukumu ya kutekeleza sheria zidi ya uhalifu mu maeneo yao. Polisi fulani banaweza kusafiri pamoya na maafisa wa uhamiaji na kubasaidia.
- Uko na haki ya kubakiya kimya.
- Uko na haki ya kukuwa na mwanasheria, na polisi inapashwa kukupatia mwanasheria kama unashukiwa kufanya uhalifu.